THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

SCHOOL BASED ASSESSMENT

KISWAHILI

SEHEMU A

Zoezi la 2

Kusoma kwa Sauti

Gredi ya 4-2026

NAKALA YA MWANAFUNZI

© 2026 The Kenya National Examinations Council

Tembo na Tumbili waliishi katika msitu wa Dunda. Tembo alifanya biashara ya kuuza matunda. Matunda hayo aliyapata kutokana na bidii yake shambani. Faida aliyopata aliitumia vyema. Alinunua shamba kubwa ili apanue kilimo cha matunda. Baada ya miaka michache, Tembo alikuwa tajiri. Alianzisha biashara nyingine ya magari ya usafiri. Alikuwa na mabasi kumi. Mabasi hayo pia yalimletea faida kubwa. Wanyama wengi walimtaka awashauri kuhusu biashara na matumizi ya pesa.

Tumbili naye aliuza hanchifu, njugu na pipi. Faida aliyopata aliitumia vibaya. Alinunua vitu vya anasa visivyo muhimu kwa maisha yake. Punde si punde, alianza kuomba pesa kwa Tembo. Ingawa Tembo alimsaidia, alimshauri abadilishe mwenendo wake mbaya.

© 2026 The Kenya National Examinations Council